**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO**

# TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA WATU WENYE ULEMAVU.

(Limetolewa kwa kuzingatia kanuni ya 8 (1)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chamwino anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya **Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.** Hivyo Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za serikali za Vijiji zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

i. Kikundi cha Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri.
ii. Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali.
iii. Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu kwa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.

CamScanner

iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kijasiriamali na

v. Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo wasiliana na Afisa Maendeleo ya jamii wa kata husika au wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo:

1. *Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa mtendaji wa Kijiji/Mtaa.*
2. *Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo,*
3. *Andiko rahisi la mradi unaoombewa Mkopo kwa kuzingatia fomu iliyondani ya mfumo na taarifa ya akaunti ya benki.*

Maombi ya mkopo yatumwe kuanzia tarehe 22/10/2025 na mwisho wa kuwasilisha maombi hay ani tarehe 22/11/2025.

Tangazo hili limetolewa na:

.............................................

Tito .P. Mganwa

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**CHAMWINO**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
CHAMWINO DISTRIC COUNCIL
P. O. Box 1126
DODOMA